**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**
**SHULE YA SEKONDARI MBEDE**

S.L.P 429,

SIMU: 0766072788/0628515375 **MPANDA**.

......./....../20......

Ndg. Mzazi/Mlezi wa

--------------------------------------------------

--------------------------------------------------

**YAH: <u>MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA</u>**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao …………………………....................………….. amechaguliwa kujiunga na kidato cha **I (KWANZA)** shule ya **Sekondari Mbede**. Unatakiwa kumleta shuleni tarehe **..............................** akiwa amekamilisha yale yote yaliyoelekezwa katika fomu hii. Muda wa kumleta mtoto ni kati ya saa mbili asubuhi na saa 7:30 mchana siku za kazi tu.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **........................** Unatakiwa kumleta mwanao shuleni kuanzia tarehe **.....................** na tarehe ya mwisho ya kuwasili ni tarehe **..................** Mtoto asipoletwa shule kati ya tarehe hizo, mzazi au mlezi utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kukamatwa na kupelekwa polisi/mahakamani.

Maelekezo mengine na fomu mbalimbali za kujaza utapata kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi alikosoma na kumaliza darasa la saba mwanao.

Aidha mzazi au mlezi unatakiwa kumsimamia mwanao na unamwezesha kupata mahitaji yake yote muda wote wa miaka mine awapo hapa shule na unawajibika kumsimamia anasoma kwa bidii kwa kukagua kazi anazofanya akirudi toka shule. Mzazi au mlezi atakaye bainika kumkatisha tamaa mtoto asisome kwa bidii na kuacha shule kwa naman yeyote atachukuliwa hatua kali za kisheria.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MBEDE**

................................
**MKUU WA SHULE.**

## MBEDE SHULE YA SEKONDARI

### MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE

**Mambo muhimu ya kuzingatia kwa anayejiunga na Shule ya Sekondari Mbede.**

a) Sare za shule:

**WAVULANA**

- Suruali mbili (02) za rangi nyeusi inatakiwa iwe inchi 21 kwenye mkunjo wa chini (turn up), isiyo bana makalio, mifuko miwili mbele (siyo kama jinsi) na mfuko mmoja kulia nyuma na iwe na rinda mbili mbele. Ukishona modo utarudishwa na ni marufuku mwanafunzi kuvaa modo na mtindo mwingine usioelekezwa.
- Pia suruali moja rangi ya damu ya mzee (**kwa wanafunzi watakaoishi bweni au hosteli**)
- Mashati mawili (02) meupe mikono mifupi.
- Fulana. Hii inapatikana shuleni.
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi (sio raba wala yeboyebo)
- Sweta rangi nyeusi "shingo ya V" (makoti hayaruhusiwi)
- Mkanda mweusi wa ngozi.
- Soksi nyeusi ndefu jozi mbili.
- Tai nyeusi yenye urefu wa kufika kwenye kitovu.

**WASICHANA**

- Sketi mbili (02) za rangi nyeusi. Inatakiwa iwe na urefu unaofika kwenye kifundo cha mguu (kisigino), Mshono wa sketi ni Rinda box iwe na mfuko mmoja kulia na zipu na huksi upande wa kushoto. Ukishona sketi za kubana utarudishwa na ni marufuku mwanafunzi kuvaa sketi ya kubana na mtindo mwingine usioelekezwa.
- Gauni rangi ya pinki mshono wa solo mpaka kwenye kisigino (**kwa watakaoishi hosteli/bweni)**
- Mashati mawili (02) meupe mikono mifupi.
- Fulana. Hii inapatikana shuleni.
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye visigino vifupi (sio raba wala yeboyebo).
- Sweta rangi nyeusi "shingo ya V" (makoti hayaruhusiwi).
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili.
- Tai nyeusi yenye urefu wa kufika kwenye kitovu.

**MUHIMU**: **Mtoto (mwanafunzi) anapokuja shuleni toka nyumbani na toka shuleni kwenda nyumbani lazima awe amevaa sare ya shule.**

b) Mavazi ya michezo

- Viatu (raba) vya michezo aina au rangi yoyote.
- Fula (Mbeya city) ya michezo
- Suruali au kaptura (Mbeya city).

***NB: Nguo zingine tofauti na zilizoainishwa katika fomu hii haziruhusiwi na hivyo mwanafunzi hatakiwi kuja nazo au kuvaa shuleni.***

c) Daftari kumi na moja (11) za Quire 3 au 2, kalamu, mkebe wa hisabati na rimu moja ya kratasi kwa ajili ya mazoezi mbalimbali shuleni.

d) Vifaa vya usafi ni Ndoo moja ndogo, Fagio la chelewa, Jembe jipya lenye mpini (kwa wavulana) na Fyekeo jipya (kwa wasichana).

e) **Mahitaji ya wanafunzi wa hosteli/bweni.**
Shule ina nafasi chache za hosteli kwa wasichana hivyo anayependa na kuhiyari mwanaye akae hosteli amlete mapema na kutoa michango yake yote kwa wakati.

i. Mahindi debe 4 (Kilo 80) kwa miezi sita (muhula)
ii. Maharage kilo 30 kwa miezi sita
iii. mchele kilo 24 kwa miezi sita
iv. Pesa shilingi za kitanzania 50,000/=
v. Maji 3000 kila mwezi.
vi. Umeme hosteli shilingi ………… kila mwezi
vii. Tochi ya betri moja au mbili
viii. Shuka mbili za bluu bahari, mto na foranya, na taulo /kitenge
ix. Sanduku imara la kuweka vitu vyake.
x. Godoro la ukubwa wa Ft $2\frac{1}{2}$ kwa Ft 6.
xi. Sahani, Bakuli, Kijiko na kikombe
xii. Ndala za kuogea
xiii. Chandarua cha pande nne na sio cha mviringo kwa juu.
xiv. Ndoo mbili zenye ujazo wa lita kumi.
xv. Mchango wa bima ya afya (Matibabu) 5000/= kwa mwaka
xvi. Fedha 7000/= kwa miezi mitatu kwa ajili ya maji. Kipimo kimoja cha maji huuzwa shilingi 1,500/= (CWSO MBEDE).

**Sheria na kanuni muhimu za Shule hii.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu.

Unanatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima;
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima;
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation);
d) Kuwahi katika shughuli za shule na nyingine utakazopewa;
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa na hasa uwapo shuleni na unaposafiri (wanafunzi wa hosteli/bweni).
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

**Makosa Yafuatayo Yanaweza Kusababisha Kufukuzwa au Kusimamishwa Shule**

a) Wizi.
b) Uasherati na ushoga.
c) Ubakaji.
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga.
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
g) Kudharau Bendera ya Taifa

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba/kusababisha mimba.
i) Kuoa au kuolewa.
j) Kutoa mimba.
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
l) Kukataa adhabu kwa makusudi.
m) Kumiliki, kutumia au kukutwa na SIMU (endapo mwanafunzi atakutwa na SIMU, simu hiyo itachukuliwa na hatarudishiwa kamwe bila kujali ni ya nani).

**Mambo mengine muhimu yanayopaswa kukamilishwa na kuwasilishwa shuleni na mwanafunzi.**

a) Medical examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali au kituo cha afya. Zahanati haziruhusiwi.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Kivuli cha cheti cha kuzaliwa.

**Form hizi zitakabidhiwa kwa Mkuu wa shule mara utakapowasili shuleni.**

**Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MBEDE**

...............................
**MKUU WA SHULE.**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**
**HALIMASHAURI YA MPIMBWE**
**SHULE YA SEKONDARI MBEDE**
**FOMU YA UTHIBITISHO NA MKATABA WA KUKUBALI KUJIUNGA NA MBEDE SHULE YA SEKONDARI**

***Makubaliano ya mkataba kati ya Mzazi, mwanafunzi na shule yatatekelezwa kama yalivyo kwa lengo la kufuta daraja sifuri na nne [division 0 and iv]***

**[A]. IJAZWE NA MWANAFUNZI:**
1. Jina kamili la Mwanafunzi ………………………………………
2. Uraia ……………………3.Dini…………………………………
4. Tarehe ya kuzaliwa …………………Wilaya………………Mkoa…..……..
5. Shule uliyohitimu elimu ya msingi …………………………………………..

Mimi ……………………………………………nikiwa na akili timamu na maarifa, nakubali kuchukua nafasi niliyopewa ya kidato cha …………… Naahidi kufuata Sheria, Kanuni, Taratibu na Masharti mengine yote ya Shule, ikiwemo kutopata alama D na 0 darasani, kutomiliki simu ya mkononi shuleni, utoro wa vipindi na kudharau baadhi ya masomo na mitihani..Endapo nitaingia kwenye makosa hayo mabaya naomba mzazi/mlezi wangu anitafutie shule nyingine na kunihamisha mara moja. Nakubaliana na hoja zilizoanishwa hapo juu na kwenye fomu ya kujiunga na shule ya Sekondari Mbede.

Jina la mwanafunzi………………………………… Sahihi ya Mwanafunzi ……………………
Tarehe ya mkataba ………………………………….

**[B]. MAELEZO BINAFSI YA MZAZI/ MLEZI ATAKAYETAMBULIWA NA SHULE**
1. Jina kamili la Mzazi/ Mlezi ……………………………………………….
2. Anuani kamili …………………………………………………
3. Kazi unayofanya ………………………………………………
4. Namba ya simu: …………………………………

Mimi ………………………………….……… Mzazi/ Mlezi wa …………………………….…

Nikiwa na akili timamu ,nimesoma (nimeelekezwa) vyema Sheria, Taratibu na Kanuni za Shule, Endapo Mwanangu ataenenda kinyume na Sheria/ taratibu za Shule na kupatikana na kosa la kumiliki simu ya mkononi shuleni, na kushiriki utoro wa vipindi, kukwepa mitihani na kudharau baadhi ya masomo, kama ilivyoainishwa hapo juu nakubali nikabidhiwe kijana wangu ili nimtafutie shule nyingine ili kuepusha madhara na majanga kwa wanafunzi wengine na niweze kumsimamia kwa karibu na sitakuwa na pingamizi ya aina yoyote juu ya jambo hili kwani nafahamu fika kwamba kilichomleta shule ni kusoma na si vinginevyo.

Sahihi ya Mzazi/ Mlezi …………………………………… Tarehe ……………………………

Taja ndugu wengine wa mwanafunzi huyu
1. ..............................................., uhusiano wake na mtoto ................................. simu .........................
2. ..............................................., uhusiano wake na mtoto ................................. simu .........................

**C. UTHIBITISHO WA AFISA ELIMU KATA MBEDE**

Jina la Afisa Elimu Kata…………………………………………

Maelekezo ya AEK ...........................................................................................................................
...................................................................................................................................................
...........................................................................................................................................
.............................................................................................................................................

Sahihi ………………………Namba ya Simu…………………………..Muhuri…………………

**MBEDE SECONDARY SCHOOL**

**SPECIAL REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

TO THE MEDICAL OFFICER
---------------------------------------------------
---------------------------------------------------
---------------------------------------------------

Name of student ----------------------------------------------------------------------------------------
Form ---------------------------- Term --------------------------- Year ---------------------------

Dear Doctor
Please kindly examine the above named student to prove his/her fitness undertaking studies at our school.

1. X-ray ( ) 2. Urine ( ) 3. Stool ( )

4. Physical fitness ( ) 5. V.D ( ) 6. Tuberculosis ( )

**A: (I) PRELIMINARY INFORMATION (BY THE STUDENT BEFORE THE DOCTOR)**

| NO | DISEASE | YES/NO | NO | DISEASE | YES/NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Tuberculosis | | 10 | Epilepsy | |
| 2 | Pneumonia | | 11 | Ear, Nose and threat | |
| 3 | Asthma | | 12 | Skin disorder disease | |
| 4 | Heart trouble | | 13 | Anemia | |
| 5 | Recurrent indigestion | | 14 | Operations | |
| 6 | Jaundice | | 15 | Serious Accident | |
| 7 | Dysentery | | 16 | Malaria | |
| 8 | Kidney and urinary trouble | | 17 | Stomach trouble | |
| 9 | Nervous breakdown | | 18 | Eye disorder | |
| 10 | Pregnancy- For a girl | | | | |

**(II) VACCINATIONS AND INNOVULATIONS HISOTRY**

| DISEASE | 1ST DATE | 2ND DATE | 3RD DATE |
|---|---|---|---|
| Small pox | | | |
| Whooping cough | | | |
| Measles | | | |
| Yellow fever | | | |
| Cholera | | | |

**Official**

**B: MEDICAL EXAMINATION REPORT**

(a) Weight

(b) Heart Beat

(c) Vision etc

**MEDICAL CERTIFICATE**
I have examined the above and consider that he/she is physically fit/unfit to undergo studies.
DOCTOR'S NAME & SIGNATURE ------------------------------------------------------------------------------

DATE -------------------------------------

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MPIMBWE**
**SHULE YA SEKONDARI MBEDE**

S.L.P 429,

SIMU: 0766072788/0765830558 **MPANDA**.

......./....../20......

Ndg. Mzazi/Mlezi wa

--------------------------------------------------

--------------------------------------------------

**YAH: MWANAO KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA**

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa mwanao ……………………….................………….. amechaguliwa kujiunga na kidato cha **I (KWANZA)** shule ya **Sekondari Mbede**. Unatakiwa kumleta shuleni tarehe **..............................** na tarehe ya mwisho ni tarehe **...................** akiwa amevaa sare za shule na amekamilisha mahitaji yote utakayoelekezwa. Mtoto asipoletwa shule kati ya tarehe hizo, mzazi au mlezi utachukuliwa hatua kali za kisheria ikiwemo kukamatwa na kupelekwa polisi/mahakamani.

**Muda wa kumleta mwanafunzi ni kati ya saa mbili asubuhi na saa 7:30 mchana siku za kazi tu.**

**MZAZI/MLEZI UNATAKIWA KUFIKA SHULENI UKIWA NA MWANAO TAREHE ............................ KUPATA MAELEKEZO YA SARE ZA SHULE NA MAELEKEZO MENGINE MBALIMBALI AMBAYO NI LAZIME UYAPATE KABLA TAREHE ZA KURIPOTI SHULE.**

Aidha mzazi au mlezi unatakiwa kumsimamia mwanao na unamwezesha kupata mahitaji yake yote muda wote wa miaka mine awapo hapa shule na unawajibika kumsimamia anasoma kwa bidii kwa kukagua kazi anazofanya akirudi toka shule. Mzazi au mlezi ukibainika kumkatisha tamaa mtoto asisome kwa bidii na kuacha shule kwa namna yoyote utachukuliwa hatua kali za kisheria ya kumnyima mtoto wako haki ya msingi ya kupata elimu.

Nakutakia usimamizi mzuri na wa karibu kwa mwanao kupata elimu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MBEDE**

...............................
**MKUU WA SHULE.**